MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA PAMOJA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018

1.0 MAPATO

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa mwaka **2017/2018** imekadiria kukusanya na kupokea jumla ya **TShs. 236,746,512,167.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ambapo jumla ya Tshs. **197,590,436,667.00** ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu, Jumla ya **Tshs.38,907,388,000.00** mapato yake yenyewe na Wahisani wanatarajiwa kuchangia **Tshs.248,687,500.00** kama inavyoonyesha katika jedwali na. 1.

Jedwali Na. 1: Makadirio ya Mapato ya Halmashauri kwa mwaka 2017/2018

NA.	CHANZO	KIASI (TSHS)	ASILIMIA
1	Mapato ya Manispaa (own source)	38,907,388,000	16.44%
	Jumla ndogo	**38,907,388,000**	
	Vyanzo vya nje:		
2	Ruzuku - Mishahara na matumizi mengineyo	103,090,104,500	43.56%
3	Fedha za maendeleo - Mifuko maalum	18,124,175,000	7.63%
4	DMDP	76,376,157,167	32.27%
	Jumla Ndogo	**197,590,436,667**	
5	Wahisani	248,687,500	0.11%
	Jumla Ndogo	**248,687,500**	
	Jumla kuu	**236,746,512,167**	

RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa mwaka **2017/2018** inategemea kupata Ruzuku kutoka Serikali Kuu jumla ya **T.shs. 197,590,436,667.00** ambazo zitatumika katika maeneo ya mishahara na utoaji wa huduma. Jedwali 2 lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa Ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Jedwali Na. 2: Ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa mwaka 2017/2018:

Mishahara		100,939,169,000
Matumizi Mengineyo		2,150,935,500
Ruzuku ya Mifuko Maalum		
Ruzuku ya maji	1,100,000,000	
DMDP	76,376,157,167	
Mfuko wa Barabara	6,431,400,000	
Livestock Fund	10,415,000	
Mfuko wa pamoja wa Afya	2,804,429,000	
Ruzuku ya Maendeleo (CDG)	2,160,610,000	
Ada ya TASAF	3,180,000,000	
Elimu bure shule za msingi	1,227,314,000	
Elimu bure shule za sekondari	1,035,320,000	
Mfuko wa maendeleo ya Jimbo	174,687,000	
Jumla Ndogo		**94,500,332,167**
Jumla Ruzuku ya Serikali kuu		**197,590,436,667**

WAHISANI

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa mwaka **2017/2018** inategemea kupata fedha kutoka kwa wahisani mbalimbali jumla ya **TShs. 248,687,500.00** ambazo zitatumika katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Wafadhili hao ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 3.

Jedwali Na. 3: Orodha ya Wafadhili:

Na.	Jina	Kiasi
1	UNICEF	248,687,500.00
	Jumla kuu	**248,687,500.00**

2.0 MATUMIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa mwaka **2017/2018** imekadiria kutumia jumla ya **Tshs. 236,746,512,167.00** katika maeneo ya Mishahara, Matumizi mengineyo na Miradi ya maendeleo.

2.1. RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU:

Kwa mwaka **2017/2018** Halmashauri itatumia jumla ya **TShs. 197,590,436,667.00** kutekeleza vipaumbele vya maendeleo na maeneo ya utoaji wa huduma, Kati ya

fedha hizo, **TShs.100,939,169,000.00** ni Mishahara ya watumishi na Kiasi cha **TShs. 2,150,935,500.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Halmashauri pia itatumia **TShs. 94,500,332,167.00** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu kupitia Mifuko Maalum.

Jumla ya matumizi kwa maeneo yakijumuisha matumizi ya kawaida, mifuko maalum, Miradi ya Maendeleo ni kama yanavyoonekana katika Jedwali Na.4 lifuatalo.

Jedwali Na. 4: Mgawanyo wa Matumizi maeneo ya Ruzuku:

Na.	Eneo la matumizi	Kiasi (Tshs)
1	Mishahara ya Watumishi	100,939,169,000
2	Matumizi Mengineyo	2,150,935,500
3	Matumizi ya fedha za mifuko maalum	94,500,332,167
	JUMLA	**197,590,436,667**

2.2. MATUMIZI FEDHA ZA NDANI-(OWN SOURCE)

Halmashauri kwa kipindi cha mwaka **2017/2018** itatumia **Tshs.38,907,388,000.00** kwa matumizi mengineyo, mishahara, miradi ya maendeleo na uchangiaji(Cost sharing). Kati ya fedha hizo **Tshs. 23,344,433,000.00** zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo na **Tshs 14,824,228,972.00** zitatumika katika maeneo ya uendeshaji wa shughuli za ofisi na **Tshs. 738,726,028.00** zitatumika katika kulipa mishahara ya watumishi.

Jedwali Na. 5 Matumizi Fedha za Halmashauri(Own Source)

NA.	MAELEZO	KIASI (TSHS)
1	Matumizi mengineyo	14,824,228,972
2	Kuchangia Miradi ya Maendeleo	23,344,433,000
3	Mishahara ya Watumishi	738,726,028.00
	Jumla kuu:	**38,907,388,000**

2.3. MATUMIZI (WAHISANI)

Halmashauri kwa mwaka 2017/2018 itatumia jumla ya **Tshs.248,687,500.00** kutoka kwa Wahisani wa UNICEF**.**

3.0 MAKADIRIO YA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018

Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imepanga kutumia **TShs.115,289,023,,667.00** kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **TShs.23,344,433,000.00** zinatokana na mchango wa Halmashauri, **TShs. 248,687,500.00** ni mchango wa Wahisani, Aidha TASAF itachangia **Tshs. 3,180,000,000.00,** ni fedha za Ruzuku ya Maendeleo na **Tshs. 88,515,903,167.00** ni fedha za mifuko maalum.

Mchanganuo wa fedha hizo kwa asilimia ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo hapa chini:

Jedwali Na. 6; MAKADIRIO YA MPANGO WA MAENDELEO

NA.	CHANZO CHA FEDHA	KIASI CHA FEDHA	ASILIMIA
1	Halmashauri	23,344,433,000	20.25
2	Ruzuku ya maendeleo (LGCDG)	2,160,610,000	1.87
3	Ruzuku ya maji	1,100,000,000	0.95
4	Mfuko wa barabara	6,431,400,000	5.58
5	Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo	174,687,000	0.15
6	Wafadhili (UNICEF)	248,687,500	0.22
7	DMDP	76,376,157,167	66.25
8	TASAF	3,180,000,000	2.76
9	Livestock Fund	10,415,000	0.01
10	Ruzuku ya elimu Bure Msingi	1,227,314,000	1.06
11	Ruzuku ya elimu Bure sekondari	1,035,320,000	0.90
	Jumla	**115,289,023,667**	100